



# TANGAZO KWA UMMA



## UUZAJI WA VIWANJA ENEO LA MADAGANYA - MOROGORO MJINI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu ya UTT, iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango; anautangazia umma juu ya uuzaji wa viwanja katika eneo la Madaganya - Morogoro Mjini. Wananchi wote mnakaribishwa kununua viwanja vyenye matumizi mbalimbali kama vile ya Biashara, Makazi, Zahanati, Viwanda, Shule na maeneo ya kuabudia.

### 1 VIWANJA VIPO.

- ❖ Kilomita tisa kwenda katikati ya mji wa Morogoro;
- ❖ Viwanja vipo mkabala na barabara kuu iendayo Iringa;
- ❖ Karibu na chuo Kikuu Mzumbe na shirika la Mzinga;
- ❖ Nusu kilomita kutoka lilipo bwawa la Mindu.

### 2 MAOMBI

- ❖ Fomu za manunuzi zinapatikana Benki ya Posta tawi la Morogoro katika jengo la Luna na matawi ya YWCA, Mkwepu na LAPF tower jijini Dar es Salaam;
- ❖ Pia fomu zinapatikana katika ofisi za UTT PID zilizopo ghorofa ya 12 katika jengo la wastaafu (Golden Jubilee Tower) mtaa wa Ohio, au kwenye tovuti ya Taasisi ya UTT ambayo ni; [www.utt.pid.org](http://www.utt.pid.org)

### 3 ULIPAJI

- ❖ Fomu zinapatikana kwa gharama ya Shs 20,000/= na mwombaji atatakiwa kulipia dhamana ya Shs. 500,000/= ambayo ni sehemu ya malipo ya kiwanja;
- ❖ Bei ya mita moja ya mraba ni Shs 7,000/= kwa viwanja vya aina zote;
- ❖ Malipo yanaweza yakafanywa katika tawi lolote la Benki ya Posta hapa nchini;
- ❖ Mwombaji, baada ya kulipa dhamana anatakiwa awe amekamilisha malipo yaliyobaki ndani ya miezi mitatu baada ya kupata ankara (invoice) ya malipo.

Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Morogoro (Kitengo cha Ardhi) au ofisi za UTT - PID Dar es Salaam, jengo la Golden Jubilee, ghorofa ya 12. Kwa mawasiliano piga simu namba 0757 254 653 / 0788 926 065 au 0717 002 954 Tembelea tovuti : [www.utt-pid.org](http://www.utt-pid.org)

## WAHI VIWANJA NI VICHACHE